# Ufadhili wa Uendelezaji wa Filamu | Mwongozo

## Ufadhili

1. Ufadhili huu unatolewa kwa watengenezaji wa filamu (waandishi / waongozaji) ambao wanakidhi vigezo vifuatavyo:

• Waliowahi kuongoza angalau filamu moja ya kutunga au makala au filamu fupi, ambayo imesambazwa nchini au kimataifa

• Awe raia wa nchi ambako wito wa maombi unafanyika,

• Anayeishi na kufanya kazi katika nchi husika.

Watayarishaji (Maprodyusa) hawastahiki kuomba.

2. Muundo wa filamu utakaokubalika kuombewa (Fomati) ni filamu za hadithi za kutunga au za makala na hata mahuluti (ya mchanganyiko kama docudrama)
(zisipungue urefu wa dakika 60)

3. Ufadhili ni kwa awamu ya maendeleo ya utengenezaji wa filamu kwa jumla. Awamu ya maendeleo ya hatua za mwanzo za filamu , lakini inaweza kuzidi, shughuli zifuatazo:

• Utayarishaji wa Mswada
• Utafiti
• Kutafiti maeneo na kutaka kujua uhusika kwa kina
• Kunadi mawazo
• Ufadhili kifedha
• Mwendelezo wa mikakati ya uuzaji na usambazaji

4. Watengenezaji filamu waliochaguliwa watapokea ruzuku ya €10,000 kwa kipindi chote cha maandalizi ya muswada wa filamu zao.

5. Ruzuku hiyo haitatolewa ikiwa shughuli zilizoainishwa kwenye mpangokazi husika zitakuwa tayari zimepokea ruzuku nyingine ndani ya muda huo wa ufadhili.

6. Kwa kipindi chote cha mwaka wa ufadhili, hairuhusiwi kushiriki au kupokea ruzuku inayofanana na hii na ambayo pia ina kipengele cha mafunzo.
Hata hivyo mfadhiliwa anaweza kushiriki warsha au mafunzo ya muda mfupi wakati wa kipindi hicho cha ufadhili bila kupokea ruzuku nyingine.

7. Miradi inayofadhiliwa lazima izingatie maadili ya Umoja wa Mataifa ya "Azimio la Haki za Binadamu" (UDHR). Miradi inayokiuka UDHR kwa, kwa mfano, kushabikia vita, kukazia unyanyasaji kimwili, kisaikolojia au kijinsia, au kukera hisia za maudhui ya kijamii au dini, haitaungwa mkono.

## Kipimo cha utayari kwa mafunzo ya DW Akademie

DW Akademie itafadhili mpangokazi wa ushauri, pamoja kutoa mafunzo ya aina mbalimbali. Watengenezaji wa filamu waliochaguliwa ni lazima wawe tayari kushiriki angalau 80% ya siku za ushauri na mafunzo yatakayotolewa.

## Mchakato wa maombi na nyaraka zinazohitajika kwa usaili

Waombaji lazima wawasilishe maombi yao kwa ukamilifu katika muda uliowekwa.

Vielelezo vinavyotakiwa kuwasilishwa kabla ya tarehe ya kufunga maombi, Oktoba 26, 2022:
• fomu ya maombi (mtandaoni)
• muhtasari wa mradi unaopendekezwa (kurasa 1-2)
• mpangokazi
• bajeti inayoonesha gharama za shughuli zilizoainishwa katika mpangokazi wa ruzuku inayoombwa

Waombaji watakaopita mchujo wa mwanzo, watatakiwa kuwasilisha mtiririko wa hadithi usiozidi kurasa 8.

DW Akademie itawasiliana na waombaji wa miradi iliyochaguliwa. Hili itafanyika takriban wiki nne baada ya tarehe ya mwisho ya kutuma maombi. Tafadhali kumbuka:

1. Maombi yasiyokamilika hayatazingatiwa.
2. Hairuhusiwi kuwasilisha maombi kwa mradi zaidi ya mmoja.
3. Hakuna sheria itakayohusu ufadhili

## Mkataba na utoaji fedha

1. DW Akademie itatoa mkataba kwa kila mtengenezaji wa filamu aliyechaguliwa.

2. Fedha za ufadhili zitatolewa kwa awamu.

3. Maelezo ya kina kuhusu ufadhili wa mradi yataianishwa katika mkataba utakaohitimishwa baada ya uteuzi kufanyika.

Hakimiliki zote za mawazo yaliyowasilishwa zitabaki kwa wamiliki asili wa haki zile. Isipokuwa kama imeainishwa vinginevyo katika mkataba.